# MAOMBI 16

## JINSI YA KUOMBA

### MAOMBI MBALIMBALI NA KUJIBIWA NA

# MUNGU

Hongera sana kwa kuokoka na kuutafuta uso wa Bwana. Kama tunavyojua tupo nyakati za mwisho, wakati ambao tunajiandaa kumpokea Mfalme na Bwana wetu Yesu Kristo, wakati ambao Yesu anakuja chukua watu wake (kanisa lake). Yesu ndiye njia pekee ya kwenda Mbinguni, yeye ni lango na Nuru pekee tunayotakiwa ikimbilia bila yeye, sisi si kitu maana yeye ni uzima wa milele.

**Mathayo 11:28 -30 ;**

> ***"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo nanyi mtapata raha nafsini mwenu kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi".***

Kitabu hiki kitakusaidia kumtwika Yesu matatizo yako kwa njia ya sala naye atakuokoa na uonevu wa nguvu za giza na kukuacha huru.Nakubariki kwa Jina la Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wa maisha yetu **Amina.**

**Mungu akubariki,**
**Petrida Karch**

# YALIYOMO


Sala ya toba na msamaha wa dhambi.............................. 4
Maombi kumuondoa shetani maishani mwetu................5
Maombi kuharibu nguvu za giza......................................6
Maombi ya Uponyaji kwa Wagonjwa...............................7
Maombi ya ulinzi wa Roho Mtakatifu...............................8
Maombi juu ya maadui zetu...........................................9
Maombi ya kuvunja madhabahu za uovu........................ 10
Maombi kujitenga na Maagano maovu ya ukoo..............11
Maombi kujiweka huru na ndoa za kipepo ...................... 12
Maombi ya kuombea siku yako.......................................13
Maombi Kufanya Agano la Damu ya Yesu Kwako ............14
Maombi ya Usiku kabla ya kulala....................................15
Maombi ya kurudisha vilivyoibiwa ...................................16
Maombi kuombea Familia zetu.......................................17
Maombi Kuombea Malango yetu ....................................18
(Uchumi,Elimu,Ajira,Ndoa,Ndoto n.k).

Maombi ya Sifa na Shukrani...........................................19

Ujumbe wangu kwako ...................................................20

## SALA YA TOBA NA MSAMAHA WA DHAMBI

Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai, Bwana Yesu ninaomba msamaha kwa dhambi zangu zote nilizotenda tangu utoto wangu hadi sasa.Ninaomba ulifute jina langu katika kitabu cha kuzimu na mauti na uliandike jina langu katika kitabu cha uzima wa milele.Ninamkana Shetani,machifu,mizimu na nguvu zote za giza. Ninakukiri na kukupokea wewe Yesu Kristo wa Nazareti uwe Bwana na mwokozi wa maisha yangu yote. Miliki maisha yangu yote,nafsi yangu na roho yangu yote sasa na hata milele.Ahsante Bwana Yesu kwa kunikomboa,kunisamehe dhambi zangu na kuniweka huru **Amina .**

Iwapo umesali sala hii kwa Imani, tambua kuwa umempokea Yesu na Yesu Kristo anaishi ndani yako (moyoni mwako). Karibu sana katika Ufalme wa Mbinguni wa (Mungu anayeishi). Kwa kumpokea Yesu umejenga mahusiano mazuri kati yako na Yesu kristo na Mungu wa Mbinguni maana kwa sala hii umepokea vitu vitatu ;

**1.Yesu Kristo.**
**2.Roho Mtakatifu.**
**3.Umekuwa mwana wa Mungu aliye hai na wewe pia ni hai.**

Usimwache Yesu endelea na wokovu, tunza vazi lako la utakatifu Kanisa li karibu nyakuliwa.

✞

# MAOMBI

## KUMUONDOA SHETANI MAISHANI MWETU

Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai, Ninajitenga nafsi yangu, roho yangu, na maisha yangu yote na mamlaka ya shetani katika ulimwengu wa mwili na roho. Imeandikwa **Yakobo 4:7;**

***"Basi mtiini Mungu,***

***mpingeni shetani,naye atawakimbia".***

Kwa jina la Yesu nakupinga shetani, nakukataa na najitenga na wewe kuanzia sasa.Najitenga na miungu mingine ya dunia hii namfuata Mungu mmoja tu naye ni **Mungu anayeishi** na si mungu wa wafu. Ewe shetani achia maisha yangu, nimemchagua Mungu wa Mbinguni na Yesu Kristo aliye hai. Naukana ufalme wako wa giza na mamlaka zako zote,najitenga na chochote kilichoniunganisha na madhabahu za giza iwe damu yangu, nguo yangu, kucha zangu,kitovu changu, nywele zangu, picha yangu au chochote kile. Ninahama ufalme wa giza na ninahamia ufalme wa Nuru wa **Mwana Kondoo Yesu Kristo** tangu sasa na hata milele. Ee Bwana Yesu ninaomba unisamehe dhambi zangu zote nilizozitenda kwa kujua au kutokujua, ninaomba ulifute jina langu katika kitabu cha kuzimu na mauti na uliandike jina langu katika kitabu cha uzima wa milele. Nimekuchagua wewe Yesu uwe Bwana, mwokozi na mmiliki halali wa maisha yangu yote sasa na hata milele **Amina.**

✞

# MAOMBI

# KUHARIBU NGUVU ZA GIZA

Kwa mamlaka ya jina la Yesu Kristo aliye hai, ninavunja nguvu zote za giza na maagano yote maovu niliyounganishwa nayo katika ulimwengu wa roho kwa kujua au kutokujua kupitia ukoo,mababu,mabibi,mizimu,vyakula au ndotoni kwa jina la Yesu.Najikomboa na kujiachilia huru kwa Damu ya Yesu. Naachia Damu ya Yesu ifute laana zote na maagano yote ya giza kinyume nami kwa Jina la Yesu.Naachia moto wa Roho Mtakatifu,uteketeze kila roho chafu zilizotumwa kunilinda na kuniweka kifungoni katika ulimwengu wa roho kwa Jina la Yesu. Nimemkabidhi Yesu Kristo maisha yangu yote, hivyo nawatangazia kukosa uhalali juu yangu. Najitenga na nguvu zote zitokazo kuzimu kwa Damu ya Yesu, nakaribisha nguvu ya ufalme wa Mbinguni ya Mungu anayeishi itawale maisha yangu yote sasa na hata milele. Nafuta jina langu, wanangu na yeyote anayenihusu kwenye madhabahu za giza kwa Damu ya Yesu, naruhusu tangu sasa jina langu ligeuzwe kuwa moto na bomu la Damu ya Yesu popote litapotajwa kwa ubaya iwe kwenye madhabahu za wachawi au waganga wakalipuliwe na kuangamizwa kwa jina la Yesu.Ahsante Bwana Yesu kwa kunikomboa na kuniweka huru na nguvu za giza **Amina.**

✞

# <u>MAOMBI</u>

# <u>UPONYAJI KWA WAGONJWA</u>

Eh Bwana Yesu ninaomba unisamehe dhambi zote nilizotenda kwa kujua au kutokujua,milango yangu ya rohoni kwa kuifungua na kumruhusu adui kupanda uharibifu na magonjwa ndani yangu. Ninaomba uzifute hati zangu zote za mashtaka zilizokuja mbele yako toka kwa adui kwa Damu ya Yako(***Damu ya Yesu***). Imeandikwa ***Isaya 53:5***;

***"Lakini alijeruhiwa kwa sababu ya dhambi zetu, aliumizwa kwa sababu ya maovu yetu,Kwa kuadhibiwa kwake sisi tumepata uhai,kwa kupigwa kwake sisi tumepona".***

Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti nakataa magonjwa na nira ya adui, nimekombolewa pale Msalabani na kuwekwa huru kwa nguvu ya ***Msalaba na Damu ya Yesu.*** Ewe ugonjwa nakukataa kwa jina la Yesu, nakuapisha kwa mamlaka ya Jina la Yesu achia maisha yangu, ng'oka na usirudi tena.Nasambaratisha madhabahu ovu,ngome, ashera,sadaka na laana zote zilizotamkwa na zilizosimamishwa kinyume na maisha yangu na afya yangu kwa Damu ya Yesu. Namfyeka kuhani wa madhabahu ovu na kumshusha kuzimu kwa jina la Yesu.Nafuta jina langu,kivuli changu na chochote kilichoshikiliwa na adui kwa Damu ya Yesu.Kwa jina la Yesu naivunja nira ya adui na kuvaa sasa nira ya Bwana Yesu nyepesi na laini. Nairuhusu Damu ya Yesu inisafishe mwili wangu wote na kuvunja vifungo vyote vya adui. Natamka uzima juu yangu sasa na hata milele, ahsante Bwana Yesu kwa kuniponya na kuniweka huru **Amina.**

# MAOMBI

## ULINZI WA ROHO MTAKATIFU

Baba katika jina la Yesu Kristo aliye hai, ninaomba ulinzi wako mtakatifu, ulinzi wako mkuu na wenye nguvu kupitia Malaika zako watakatifu na Roho wako Mtakatifu.Imeandikwa katika Neno lako **Zaburi 91:11**

***"Maana Mungu atawaamuru Malaika wake,wakulinde popote uendapo".***

Kwa jina la Yesu Kristo aliye hai ninaachia ulinzi wa Roho Mtakatifu katika safari yangu yote niishiyo hapa duniani, uchumi wangu, ndoa yangu, watoto wangu, shule yangu n.k. Roho Mtakatifu nakuruhusu ng'oa,haribu,bomoa, angamiza na uteketeze nguvu zote za giza zilizotumwa kuniharibia hatima na maisha yangu. Roho Mtakatifu futa kila mipango na michoro miovu iliyopangwa sirini kinyume na maisha yangu kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti. Naachia Moto wa Roho Mtakatifu uangamize na kuteketeza kambi zote za adui zilizojiinua kupigana nami, natuma moto wa Roho Mtakatifu uteketeze madhabahu zote ovu za adui kinyume nami hadi majivu pamoja na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu ukachinje makuhani wote na roho zote chafu kwa jina la Yesu. Najifunika na Damu ya Yesu maisha yangu yote sasa na hata milele,Nawaruhusu Malaika wa Bwana mnilinde popote niendapo na niingiapo na Damu ya Yesu inifunike maisha yangu yote **Amina**.

✞

# MAOMBI
# JUU YA MAADUI ZETU

Kwa jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, Bwana Yesu ninawaleta adui zangu wote mbele zako kama Neno lako la Ufalme linavyosema katika kitabu kitakatifu **Kutoka 14:14,**

***"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya".***

Adui zangu wote, adui wa ndoa, uchumi, kesho yangu, wanangu, na wote wanaonisumbua na kunitesa katika ulimwengu wa mwili na wa roho.Ninawakabidhi wote kwa Bwana,ninakuomba Bwana uwapige kwa niaba yangu *"**maana wewe utapigana na adui zangu wote nami nitanyamaza kimya".*** Enyi adui zangu wote mliojiinua kinyume nami, adui rafiki, mchawi, mganga, msoma nyota au mfalme wa giza nawaamuru mdondoke chini, mvunjike, msambaratike na muachie maisha yangu yawe huru kwa mamlaka ya jina la Yesu Kristo. Ninawashinda kwa Damu ya Mwana Kondoo/Damu ya Yesu na nawaondolea umiliki na uhalali maishani mwangu sasa na hata milele.Najitenga nanyi kwa moto wa Roho Mtakatifu na Damu ya Yesu. Natuma Moto wa Roho Mtakatifu uharibu kazi zenu,vitendea kazi vyenu na kila mpango mbaya mlioupanga kinyume na maisha yangu kwa jina la Yesu. Nawatangazia kushindwa na kudondoka kwenu sasa na hata milele kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti **Amina.**

✞

# MAOMBI

## KUVUNJA MADHABAHU ZA UOVU

Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai, Najitenga nafsi yangu, roho yangu, maisha yangu yote, uzao wangu na madhabahu zote ovu zilizojengwa kinyume nami.Natengua kila kafara au sadaka iliyotolewa kinyume na maisha yangu katika madhabahu hizo kwa jina la Yesu.Natuma radi ya Bwana ikabomoe na kuteketeza madhabahu zote ovu,ikavunje kila nguzo na ashera zilizosimamishwa kinyume nami kwa jina la Yesu.Natuma Malaika Watakatifu wapite kila eneo, walinzi wa kipepo waliotumwa kunifunga na kunilinda katika ulimwengu wa roho muwakamate,muwafunge pingu na kuwateketeza kwa moto wa Roho Mtakatifu hadi majivu kwa jina la Yesu Kristo,Imeandikwa katika Neno lako ***Ufunuo 12:11;***

***"Nao wakamshinda kwa Damu ya mwanakondoo, na kwa neno la ushuhuda wao,ambao hawakupenda maisha yao hata kufa".***

Kwa jina la Yesu, nazishinda na kuzibomoa madhabahu zote ovu zilizojengwa kinyume nami kwa Damu ya Yesu. Nafuta laana zote chafu kwa Damu ya Yesu na ninairuhusu Damu ya Yesu inene mema sasa juu yangu na maisha yangu yote.Ninajiweka huru sasa na hata milele toka madhabahu zote ovu kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti **Amina.**

✞

# MAOMBI

## KUJITENGA NA MAAGANO MAOVU YA UKOO

Baba katika jina la Yesu kristo wa Nazareti aliye hai, Ninajitenga leo na maagano yote ya miungu migeni katika ukoo wangu niliyounganishwa nayo kupitia mababu,mabibi, wazazi kwa kujua au kutokujua kwa jina la Yesu. Maagano yote ya miungu,mizimu,uchawi,uganga niliyounganishwa nayo nayakana leo kwa jina la Yesu. Nakomboa chochote changu kilichounganishwa na maagano hayo iwe damu,kitovu,jina langu,uzao wangu, kwa Damu ya Yesu.Naachia upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu na Damu ya Yesu ikate kila cheni niliyounganishwa nayo katika ulimwengu wa Roho kwa jina la Yesu.Natengua kila sadaka na kafara zilizotolewa kwa miungu migeni kinyume nami kwa jina la Yesu.Nakomboa kitovu changu na kufuta kila laana ovu zilizotamkwa kinyume nami kwa Damu ya Yesu. Kwa jina la Yesu nachagua baraka nakataa laana zote zinazonifuatilia kupitia wazazi wangu, mababu zangu au ukoo wangu kwa jina la Yesu.Naruhusu Damu ya Yesu ipite mwilini mwangu,nafsini mwangu na kufuta kila laana, kila agano,kila alama,kila magonjwa ya kurithi,mabalaa,nuksi na kuachia umiliki wa Yesu Kristo ndani yangu sasa na hata milele. Ninahama familia za miungu migeni na kuamia familia ya Yesu Kristo wa Nazareti. Ahsante Bwana Yesu kwa kunikomboa na kuniweka huru **Amina**

✞

# MAOMBI

## KUJIWEKA HURU NA NDOA ZA KIPEPO

Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai, ninajitenga na ndoa zote za kipepo katika ulimwengu wa roho nilizounganishwa nazo kwa kujua au kutokujua.Mahusiano ya kiroho niliyounganishwa nayo ndotoni bila ridhaa yangu nayavunja leo kwa jina la Yesu. Yeyote aliyejiunganisha nami kimahusiano bila ridhaa yangu katika ulimwengu wa roho najitenga naye kwa Jina la Yesu. Ninajitenga na kujifarakanisha na majini mahaba katika ulimwengu wa roho kwa jina la Yesu. Ninaivua pete ya ndoa ya kipepo katika ulimwengu wa roho na vitu vyote nilivyopewa kama zawadi navikusanya vyote na kuvichoma na moto wa Roho Mtakatifu kwa jina la Yesu. Kwa jina la Yesu, ninakichana na kukiteketeza cheti cha ndoa ya kipepo kwa moto wa Roho Mtakatifu.Naachia upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu na kumfyeka jini mahaba na uzao wake wote, natamka vifo juu yenu na kuwaseta kuzimu kwa jina la Yesu. Ninaivunja nira ya adui na kuivaa nira ya Bwana iliyo nyepesi na laini sasa na hata milele kwa jina la Yesu.Ninairuhusu Damu ya Yesu isafishe malango yangu yote, maisha yangu yote na kuyaweka huru sasa na hata milele. Nakuruhusu Bwana utawale na kumiliki maisha yangu yote sasa na hata milele na ninakuruhusu Roho Mtakatifu uishi ndani yangu na kutumia mwili wangu kuwa hekalu lako safi na Takatifu kwa Jina la Yesu. Ahsante Bwana Yesu kwa kunikomboa na kuniweka huru na ndoa za kipepo ***Amina.***

## MAOMBI YA ASUBUHI KUOMBEA SIKU YAKO

Bwana wangu na Mungu wangu uketiye mahali pa juu,ninakushukuru kwa kunilinda usiku kucha na kunipa kibali tena cha kuiona siku ya leo. Baba ninasema ahsante kwa upendo na kwa kunipa pumzi leo tena,na kunipa nafasi nami kuwa mmojawapo wa wanaoendelea kuishi hapa duniani.

Ninaikabidhi siku yangu yote ya leo mikononi mwako,ninaomba Bwana Yesu uniongoze wewe,niingiapo na kutoka Damu yako inifunike.Nafunga kuzimu,mauti,uharibifu,kifo na kila uovu wa adui uliopangwa kinyume nami kwa siku ya leo, natangaza hauna nafasi juu yangu kwa jina la Yesu. Kila mitego na michoro miovu iliyotegwa kinyuma nami na nyumba yangu siku ya leo, ninaiharibu na kuisambaratisha kwa Damu ya Yesu. Kila laana zilizoachiliwa na kunena uovu juu yangu, ninazinyamazisha kimya kwa Damu ya Yesu. Ninawaruhusu Malaika watakatifu wa Bwana,wanilinde siku ya leo kila ninapoenda,ninapoingia na kutoka kwa jina la Yesu. Navitakasa na kuvibariki vinywaji pamoja na vyakula vyote nitavyokula siku ya leo kwa Damu ya Yesu.Natamka ushindi,baraka,mafanikio,furaha,afya na kila mema yakawe upande wangu na ninayapokea siku ya leo kwa jina la Yesu.Ahsante Bwana Yesu kwa kunipenda,kunilinda na kunipa Malaika wako watakatifu wanilinde siku ya leo **Amina.**

✞

# MAOMBI

## KUFANYA AGANO LA DAMU YA YESU KWAKO

Eh! Bwana Yesu nimekuja mbele zako sasa ili nipate kutengeneza nawe Bwana wangu. Ninaomba toba na rehema yako kwa uovu wote ulionitangulia wa wazazi, ukoo, mababu, mabibi na kila maagano maovu yaliyofanya kabla yangu toka kizazi cha kwanza hadi sasa. Baba ninaomba nisamehe kwa kukushirikishwa na kuunganishwa na uovu huo na leo hii agano hilo ovu linanifatilia mimi na uzao wangu na kutesa maisha yangu yote. Imeandikwa katika kitabu chako kitakatifu ***Maombolezo 5:7;***

***"Wazee wetu walitenda dhambi na hawapo tena,nasi tunateseka kwa sababu ya makosa yao."***

Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai,najitenga ,natengua na kuvunja maagano yote ya ukoo, miungu migeni na kila viapo vilivyofanyika kinyume na Mungu aliye hai.Kila kafara,sadaka na matambiko yaliyofanyika kinyume na Ufalme wa Mbinguni nayavunja na kujifarakanisha nayo kwa Damu ya Yesu. Ninainyamazisha damu yoyote iliyomwagwa kama sadaka kushirikia agano hilo ovu kwa Damu ya Yesu. Nakata cheni zote,vifungo vyote na kudondosha ufalme huo,nguzo,ngome na ashera zote zinazoshilikia agano hilo kwa jina la Yesu. Ninafanya Agano jipya sasa la Damu ya Yesu kwenye malango yangu,uchumi wangu, uzao wangu na kila kinachonihusu. Ninairuhusu Damu ya Yesu inene mema juu yangu na kila kinachonihusua sasa na hata milele, ahsante Bwana Yesu kwa kuniweka huru,kunisamehe na kufanya agano nami la Damu yako la milele **Amina.**

✞

# MAOMBI

## YA USIKU KABLA YA KULALA

Bwana wangu na Mungu wangu uketiye mahali pa juu,Mfalme wa amani na Mungu mwenye nguvu Alfa na Omega,ninakushukuru kwa ulinzi wa siku ya leo yote. Baba ninasema ahsante kwa upendo, ulinzi wako kwangu tangu asubuhi,mchana na hata sasa usiku ninapoenda kupumzika. Ninaomba toba na rehema kwa dhambi zangu zote nilizozitenda siku ya leo kwa kuwaza,kunena,kutenda, dhambi ninazozikumbuka na hata zile dhambi nisizozikumbuka pia. Ninaomba ulifute jina langu katika kitabu cha kuzimu na mauti na uliandike jina langu katika kitabu cha uzima wa milele. Ninafuta hati zote za mashtaka kinyume nami kwa Damu ya Yesu na kuzichoma kwa moto wa Roho Mtakatifu hadi majivu kwa jina la Yesu. Ninadondosha nguzo zote za uovu adui alizozisimamisha kinyume nami siku ya leo kwa jina la Yesu. Ninafunga giza,kuzimu na mauti haina mamlaka juu yangu usiku wa leo kwa jina la Yesu. Ninayaosha malango yangu yote ya ndoto na kuyafunika kwa Damu ya Yesu. Ninafunga ndoto zote chafu zitokazo kwa adui hazina nafasi kwangu,naziruhusu ndoto safi na nzuri tu zitokazo kwa Bwana usiku wa leo kwa jina la Yesu. Enyi adui zangu wote, wachawi, waganga na maumbo yenu yote maovu mtumiayo kufanya uovu ninawafunga hamtafanikiwa kwa jina la Yesu. Ninazama ndani ya bahari ya Damu ya Yesu usiku kucha pamoja na watoto wangu na vyote vyangu kwa jina la Yesu. Ahsante Bwana Yesu kwa kunilinda **Amina.**

✞

## MAOMBI
## KURUDISHA VILIVYOIBIWA

Kwa jina la Yesu Kristo mwana wa Mungu aliye hai. Natumia mamlaka ya jina la Yesu kuviita na kuvirudisha vyote nilivyoibiwa katika ulimwengu wa roho.Ninaiita nyota yangu popote ilipoibwa na kufichwa njoo kwa jina la Yesu (Nyota yangu njoo kwa jina la Yesu × 4).Nakiita chochote changu kilichoibiwa na kufichwa kwenye madhabahu za wachawi,waganga, freemasons au kuzimu zote duniani njoo unirudie kwa jina la Yesu. Navunja na kuharibu kila kafara iliyotolewa kinyume na mimi kama agano la kushikilia vitu vyangu kwa jina la Yesu. Natumia Damu ya Agano, Damu ya Yesu kufuta na kunyamazisha kila sauti ya damu ya kafara inayonena mauti, kifo na uharibifu juu yangu, inyamaze kimya na ifutike kwa Damu ya Yesu.

Nashinda nguvu zote za uovu kwa jina la Yesu.Nimemchagua Yesu Kristo maishani mwangu, hivyo nipo huru na nguvu zote za giza.Shetani na mawakala zako, nawanyang'anya maisha yangu na vitu vyangu vyote vinavyonihusu kwa jina la Yesu Kristo. Ninawatuma Malaika wa Bwana mfuate vitu vyangu vyote vilivyoibwa na mnirudishie kwa jina la Yesu.Nakataa chochote changu kutumika kwenye ufalme wa giza bali vitumike kwa kusudi la Bwana na ufalme wake wa Nuru ulio juu.Ahsante Bwana Yesu kwa kunisaidia, kunirudishia na kunipatia tena haki yangu iliyoibiwa **Amina.**

✞

# MAOMBI

# KUOMBEA FAMILIA ZETU

Mungu wetu uketiye mahali pa juu,Alfa na Omega, ninakushukuru kwa upendo wako ulio nao kwetu sisi wanadamu.Baba ninaileta leo familia yangu yote kwako (watoto,ndugu,wazazi) wangu tunaomba toba na rehema kwa makosa na uovu wote tulioshitakiwa mbele zako tangu kizazi cha kwanza hadi sasa.Tunatubu kwa maagano yote ya miungu migeni iliyounganishwa nasi kwenye familia yetu na mababu na mabibi kwa kujua au kutokujua na leo maagano hayo yakiendelea kuitesa familia yetu.Tunaomba toba,rehema na ukombozi wako Bwana.Tumekosa Baba,tunaomba utusamehe,tumeijua kweli na tunachagua sasa baraka na kuikataa laana. Tunajitenga na kuikana miungu yote migeni iliyoungamana nasi na kutumiliki katika ulimwengu wa roho kwa jina la Yesu.Tunavunja nguvu zote za sadaka za miungu inayotumiliki na inayotushikilia kwa Damu ya Yesu. Tunanyamazisha damu zote zilizomwagika kama sadaka kwenye madhabahu za uovu zinazonena ,kifo,magonjwa,mauti au laana juu ya familia yetu kwa Damu ya Yesu. Tunairuhusu Damu ya Yesu inene mema, afya,baraka,mafanikio,uzima na uhai juu yetu sasa na hata milele kwa jina la Yesu. Tunaikabidhi familia yetu yote kwako Bwana na tunakuruhusu uimiliki na uitawale sasa na hata milele.Tunalifunika lango la familia yetu kwa Damu ya Yesu, tunaruhusu amani,upendo ,ushirikiano na wewe Bwana uishi na utawale daima ndani yetu **Amina.**

✞

# MAOMBI

## KUOMBEA MALANGO YETU

### (UCHUMI,ELIMU,AJIRA,NDOA,NDOTO & BARAKA)

Bwana Yesu nakushukuru kwa upendo wako kwangu, ahsante kwa uzima, uhai na ulinzi unaonilinda kila siku.Nayakabidhi malango yangu yote ya rohoni kwako lango la uchumi,ajira,ndoa,kazi,elimu,ndoto,baraka pamoja na malango yangu yote ya rohoni makubwa na madogo kwa jina la Yesu. Imeandikwa katika Neno lako ***Yoshua 1:5;***

***"Hakuna mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe,sitakupungukia wala sitakuacha"***

Kwa jina la Yesu, adui yeyote aliyesimama mbele ya malango yangu kwa lengo la kunipinga,kushindana nami,kunizuia au kunichelewesha nisiifikie hatima yangu nzuri, ninaachia upanga wa Bwana umfyeke na kumshusha kuzimu kwa jina la Yesu. Nafuta laana na sauti zote ovu zinazonena uharibifu juu yangu kwa Damu ya Yesu. Nabomoa na kusambaratisha madhabahu zote ovu pamoja na sadaka zilizosimamishwa kinyume na maisha yangu kwa jina la Yesu.Ninairuhusu Damu ya Yesu isafishe na kunena mema juu ya malango yangu yote kwa jina la Yesu.Nafunga kuzimu,giza na mauti havina mamlaka juu ya malango yangu yote tangu sasa na hata milele.Kila kilichofungwa kwenye malango yangu na adui nakifungua sasa na kukiweka huru kwa jina la Yesu.Nayafunika malango yangu yote kwa Damu ya Yesu na kuruhusu Malaika wa Bwana wayalinde **Amina.**

✞

# MAOMBI YA SIFA NA SHUKRANI

Mungu wangu na Baba yangu mwema,ninakuinua juu wewe uliye Alfa na Omega,Mwanzo na Mwisho,utukufu,heshima na enzi ni zako pia milele na milele.Ninakusifu,ninakutukuza,ninasujudu mbele ya ukuu wako,ninakuinua juu kuliko mbingu zote, ninakupa heshima maana wastahili kuheshimiwa pokea sifa zangu kutoka katika kilindi cha moyo wangu. Ni upendo wa ajabu ulio nao kwangu Bwana ,ulikubali kushuka duniani na kuchukua mwili wa unyonge ili unikomboe na unirudishe tena katika enzi yako ya milele.Ninakushukuru Baba yangu na Mungu wangu Mtakatifu kwa kunipenda,kunikomboa toka utumwa wa dhambi, ninaungana na Malaika wote wa mbinguni kukuabudu,kukutukuza,kukusifu na kuliinua juu jina lako,maana hakuna jina lingine lenye Mamlaka,nguvu,utiisho na liwezalo kutukomboa isipokuwa jina lako. Mungu Mtakatifu uketiye mahali pa juu ,ninaahidi kwako Baba yangu sitachoka kukusifu,kukuabudu,kukushukuru,kukutukuza na hata kukutangaza pote duniani hadi pumzi yangu ya mwisho itakapotoweka,nitaendelea kulitaja jina lako kila niingiapo na nitokapo.Roho Mtakatifu,mwalimu wangu mzuri uwe nami siku zote katika safari yangu niwapo hapa duniani maana pasipo wewe hatuwezi kitu. Baba ninakushukuru kwa baraka ulizonijalia na unazoendelea kunijalia pamoja na uhai unaonipatia kila siku. Ahsante Bwana Yesu, Mfalme wangu na Mungu wangu **Amina.**

## UJUMBE WANGU KWAKO

Soma sana Neno la Mungu (Biblia), funga, Sali sana, tenda matendo mema, sikiliza mahubili ya Mungu anayeishi kwa watumishi wake wa kweli na utunze vazi lako la utakatifu.Nakutakiwa baraka nyingi na ushindi mkubwa katika safari yako ya wokovu **.**

Kanisa la Bwana li karibu kunyakuliwa, unabii umetimia, usimwache Bwana Yesu ishi maisha ya utakatifu ili uwe mmojawapo katika wateule /watakatifu wanaotarajia kunyakuliwa**.**

***Iwapo umeguswa na huduma hii,unaweza changia sadaka yako ili tuprint vitabu vingi na wengine wapokee uponyaji na kufikiwa na wokovu bure kama ulivyofikiwa wewe ili nao wauingia Ufalme wa Mbinguni na Bwana apate nyakua mavuno mengi siku ya unyakuo.*** Changia sadaka yako kwa number hizi;

***Jina: Jesus Christ Ambassadors***
***M-Pesa: 0755734678( Waliopo Tanzania)***
***M-Pesa: +255755734678( Waliopo nje ya Tanzania)***
***Lipa kwa M- Pesa: 5495860***
***Lipa kwa Tigo pesa: 5660346***

Bwana akubariki sana,akuongezee ulipopunguza na akumbuke hazina yako ya Mbinguni **Amina.**

**Mwandishi wa kitabu;**
**Petrida Karch**
**Email: petridakarch@gmail.com**
**+491758114293**